# K.P.S.E.A
# TATHMINI YA SHULE YA MSINGI
# TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA 2, 202
# GREDI YA 4 - KISWAHILI INSHA
# Muda: Dakika 40

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina: ______________________________ Shule: ______________________________

Nambari ya Tathmini: ______________________________ Tarehe: ______________________________

Nambari ya Shule: ______________________________ Sahihi: ______________________________

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mthani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Andika tarehe,nambari ya shule yako kisa weka sahihi yako.
3. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
4. Andika insha kama ulivyoelekezwa.

JEDWALI LA ALAMA

| SEHEMU | INSHA | LUGHA | KUSI/KUZU | ASILIMIA (%) | KUZ 1 | KUZ 2 | KUF 1 | KUF 2 | KUK 1 | KUK 2 | CHI 1 | CHI12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA ALAMA | ALAMA 20 | ALAMA 30 | ALAMA 30 | | 90-100 | 75-89 | 58-74 | 41-57 | 31-40 | 21-30 | 11-20 | 1-10 |
| POINTI | | | | | 8 POINTI | 7 POINTI | 6 POINTI | 5 POINTI | 4 POINTI | 3 POINTI | 2 POINTI | 1 POINTI |
| JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | | | | | | | | | | |

## SEHEMU A: UFAHAMU
**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako. (alama 20)**

**Andika insha kuhusu**

**<u>SHEREHE YA KUFANA</u>**

### HUU NDIO UKURASA WA MSWISHO ULIOPIGWA CHAPA

***MWONGOZO WA KUSAHISHA***

***MFANO WA INSHA: SHEREHE YA KUFANA***

Ilikuwa siku ya Jumamosi tulivu. Jua lilichomoza kwa tabasamu likiashiria kuwa siku hiyo ingekuwa ya kipekee. Familia yetu ilikuwa imejiandaa vilivyo kusherehekea siku ya kuzaliwa ya kaka yangu mkubwa, Baraka. Maandalizi yalianza mapema alfajiri huku kila mmoja akijitolea kwa hali na mali.

Uwanja wa nyumbani ulipambwa kwa mapambo ya rangi mbalimbali. Mapululizo mekundu, ya bluu na ya manjano yalining'inia kila mahali yakicheza na upepo mwanana. Katikati ya meza kuu, kulikuwa na keki kubwa iliyopakwa rangi ya chokoleti na kuandikwa jina la Baraka kwa herufi za dhahabu. Harufu nzuri ya pilau na nyama choma ilitanda hewani na kutufanya sote tuchuruzike mate.

Wageni walianza kuwasili mwendo wa saa nane mchana. Walikuwa wamevalia mavazi yao ya sikukuu yaliyopendeza ajabu. Sherehe ilianza kwa maombi na nyimbo za kumshukuru Mungu. Baada ya hapo, mziki mwororo ulianza kuchezwa na wageni wakajumuika pamoja kwa furaha na vicheko. Baraka alionekana mchangamfu sana huku akipokea zawadi nyingi kutoka kwa marafiki na jamaa.

Wakati wa kukata keki ulipowadia, sote tulisimama na kuimba wimbo wa "Heri ya Kuzaliwa". Baraka alikata keki na kutulisha sote kwa upendo. Baada ya hapo, tulipakuliwa vyakula vitamu na vinywaji baridi. Kila mtu alikula na kusaza. Hakika ilikuwa karamu ya kukata na shoka ambayo sitaisahau kamwe.

Sherehe ilitamatika jioni huku wageni wakiondoka mmoja baada ya mwingine. Kila mmoja aliondoka akiwa na tabasamu tele usoni. Siku hiyo ilibaki kuwa kumbukumbu muhimu moyoni mwangu kwani ilitunidhihirishia umuhimu wa upendo na umoja katika familia.

***MWONGOZO WA KUSAHIHISHA (ALAMA 20)***

Mwalimu/Mtahini anapaswa kuzingatia vigezo vifuatavyo wakati wa kutuza alama:

**1. Maudhui (Alama 04)**
- Je, mwanafunzi amezingatia kichwa cha insha (Sherehe ya Kufana)?
- Je, kuna mtiririko mzuri wa mawazo (mwanzo, katikati na mwisho)?

**2. Msamiati (Alama 04)**
- Matumizi ya maneno mwafaka yanayohusiana na sherehe (mfano: karamu, pambo, mgeni, zawadi).
- Matumizi ya tamathali za usemi kama tashbihi au methali (mfano: *karamu ya kukata na shoka*).

**3. Sarufi na Hijai (Alama 04)**
- Usahihi wa tahajia (spelling) ya maneno.
- Matumizi sahihi ya nyakati na viambishi.

**4. Alama za Uandishi (Alama 04)**
- Matumizi sahihi ya herufi kubwa, mkwaju, kitone, na alama za nukuu.

**5. Ubunifu na Mpangilio (Alama 04)**
- Hati nadhifu na inayosomeka.
- Urefu wa insha (isiwe fupi sana au ndefu kupita kiasi).

| Alama (20) | Pointi | Kiwango cha Mafanikio |
|---|---|---|
| 18 – 20 | **8** | Anazidi Matarajio |
| 15 – 17 | **7** | Anazidi Matarajio |
| 12 – 14 | **6** | Anafikia Matarajio |
| 09 – 11 | **5** | Anafikia Matarajio |
| 07 – 08 | **4** | Karibu Kufikia Matarajio |
| 05 – 06 | **3** | Karibu Kufikia Matarajio |
| 03 – 04 | **2** | Chini ya Matarajio |

| | | |
|---|---|---|
| 01 – 02 | **1** | Chini ya Matarajio |